MTIHANI WA MUHULA KATI 2018

DARASA LA NNE

KISWAHILI
SEHEMU YA
KWANZA:
LUGHA

Muda: Saa 1 dakika 40

LUGHA

Soma kifungu kifuatacho, kina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila pengo umepewa majibu manne. Jaza kila pengo kwa jawabu lifaalo zaidi.

Siku ___1___ mama ___2___ na mimi tulifunga safari ___3___ kwenda sokoni kununua matunda ___4___ . Tulipokuwa ___5___ tukielekea sokoni tulishuhudia kisa cha ajabu, tulikutana na mzee mmoja aliyekuwa ___6___ punda wake mabegani.

___7___ tulisimama na kushangaa sana kumwona mzee kama ___8___ amejibebea mzigo huo wa ___9___ . Mzee alipoulizwa sababu ___10___ tukio hilo, hakuwa na ___11___ la kusema ila kutikisa ___12___ chake tu. Alitokezea mvulana mmoja aliyesimama mbele ya mzee huyo ___13___ kumwambia amweke punda huyo ___14___ ama alazimishwe kufanya ___15___ .

1. A. mmoja B. kimoja C. mamoja D. moja
2. A. wangu B. angu C. yangu D. changu
3. A. wa B. ya C. za D. la
4. A. mabivu B. bivu C. mbivu D. vibivu
5. A. jiani B. njiani C. njia D. jia
6. A. amekibeba B. ameubeba C. amembeba D. wamembeba
7. A. Sote B. Wote C. Vyote D. Pote
8. A. hiyo B. huyo C. huo D. hao
9. A. achabu B. anjabu C. ajabu D. aajabu
10. A. za B. wa C. la D. ya
11. A. yeyote B. wowote C. lolote D. chochote
12. A. mgongo B. kichwa C. tumbo D. magoti
13. A. na B. cha C. la D. wa
14. A. juu B. kando C. ndani D. chini
15. A. hivyo B. hio C. hiyo D. hicho

...nakala bila idhini kwa

Kutoka swali la 16 hadi 30, chagua jibu kulingana na maagizo.

16. Kamilisha kwa sifa sahihi:
Darasa hili ni__________sana.
A. dogo
B. ndogo
C. kidogo
D. mdogo

Andika sentensi ifuatayo katika wingi.

17. Chura ameruka mtoni.
A. Chura wameruka mtoni.
B. Vyura wameruka mitoni.
C. Vyura vimeruka mitoni.
D. Machura yameruka mitoni.

18. Kamilisha salamu kwa usahihi:-
Shikamoo?
A. Nzuri
B. Njema
C. Marahaba
D. Jaala.

19. **Kamilisha kitendawili kifuatacho:-**
Babu analilia msituni.
A. Ndege
B. Mtema kuni
C. Mtoto
D. Shoka

20. Neno **kipepeo** huwa katika ngeli gani?
A. KI-VI
B. U-I
C. A-WA
D. LI-YA

21. Jiko la makaa huitwa:-
A. seredani
B. sebule
C. shubaka
D. meko

Tumia kiulizi sahihi:

22. Kitabu _______ kilichoraruka?
A. kigani
B. ngapi
C. gani
D. upi.

23. Taja jina la umbo hili.



A. mraba
B. mstatili
C. mche
D. mduara

24. Teua sentensi iliyo katika wakati timilifu.
A. Mwanafunzi anacheza kandanda.
B. Magari yameendeshwa kwa utaratibu.
C. Kalamu ilinunuliwa jana.
D. Redio itaimba wimbo.

25. Mzazi wa kiume wa baba au mama ni:-
A. babu
B. nyanya
C. dada
D. kaka.

26. Kanusha: Mwalimu anaandika ubaoni.
A. Mwalimu ameandika ubaoni.
B. Walimu hawaandika ubaoni.
C. Mwalimu hakuandika ubaoni.
D. Mwalimu haandiki ubaoni.

27. Matunda ______ ni ya mwalimu.
A. hili
B. hizi
C. haya
D. hawa

28. 999 kwa maneno ni:-
A. Mia tisa na sita.
B. Elfu tisa na tisini na tisa.
C. Mia sita na sitini na sita.
D. Mia tisa na tisini na tisa.

29. Kamilisha methali ifuatayo:
Mtoto akililia wembe:-
A. ficha
B. mpe
C. nunua mwingine
D. tupa.

30. Yupi si ndege?
A. Ngiri
B. Mbayuwayu
C. Korongo
D. Kipanga

Compiled and supplied online by Schools Net Kenya | P.O. Box 85726 – 00200, Nairobi |
Mob. 0711 8822 27 | Email: infosnkenya@gmail.com | Order answers online at www.schoolsnetkenya.com

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 hadi 40.

Usafi wa mazingira ni jambo ambalo linafaa kutiliwa maanani na wote. Kwanza kabis nini maana ya neno **mazingira**; mazingira ni ile hali inayokizunguka kiumbe chochote. Kw hivyo, chochote kilicho karibu na binadamu au mnyama yeyote ni mazingira na ni lazim kama ibada watu kuishi katika mazingira safi.

Katika kusafisha mazingira, ni lazima kila sehemu isafishwe kuanzia katika nyumb hadi nje ya nyumba bila kusahau usafi wa mwili pia. Hii ni kwa sababu kuna wale utakaowaon wakiwa safi na nadhifu kimwili lakini uingiapo katika nyumba zao basi ndipo utakapojua kuw hawazingatii usafi katika nyumba zao.

Tunapozungumzia nyumba, si katika **sebule** tu bali pia hata katika chumba cha malaz na jikoni. Mwanzo kabisa, kupikiwako chakula hutakikana daima dawamu kuwa safi la si hivy huenda kukasababisha maradhi mbalimbali kama vile: kipindupindu na homa ya matumbo n magonjwa mengineyo yanayosababishwa na mazingira machafu.

Sote tuungane pamoja na kuhakikisha kwamba mazingira yetu ni safi kwa njia zote.

31. Ni kwa nini usafi wa mazingira ni muhimu?
- A. Husababisha magonjwa
- B. Watu wengi hupenda mazingira machafu
- C. Mazingira safi hayapendezi
- D. Huzuia magonjwa mbalimbali

32. Kulingana na ufahamu, nini maana ya neno **mazingira**?
- A. Nyumbani kwa binadamu.
- B. Hali isiyosababisha ugonjwa.
- C. Hali inayokizunguka kiumbe.
- D. Mahali palipo na uchafu mwingi.

33. Watu na wanyama wanashauriwa kuishi katika mazingira:-
- A. machafu
- B. safi
- C. masafi
- D. chafu

34. Unaposafisha mazingira lazima:-
- A. usafishe sehemu zote
- B. usisafishe sehemu zote
- C. usafishe mwili pekee
- D. usafishe jikoni pekee.

35. Watu wengine huwa safi katika mwili lakini:-
- A. nyumba zao ni chafu
- B. nywele zao hazijachanwa
- C. nguo zao hazijafuliwa
- D. nyumba zao ni safi.

36. Neno **sebule** limepigiwa mstari, lina maana gani?
- A. Hali ya kuwa safi.
- B. Usafishaji wa mwili.
- C. Chumba cha upishi.
- D. Chumba cha kupokelea wageni.

37. Ni sehemu ngapi za nyumba zinazotakikana kusafishwa?
- A. Mbili
- B. Moja
- C. Zote
- D. Nne

38. Ni maradhi gani yanayosababishwa na uchafu?
- A. Malaria
- B. Kipindupindu
- C. UKIMWI
- D. Malale

39. Katika aya ya mwisho, tunaambiwa ya kwamba:-
- A. tuungane kusafisha mazingira
- B. tuungane kusafisha jikoni
- C. tusiungane kusafisha mazingira
- D. tusiungane kusafisha jikoni

40. Yape makala haya kichwa?
- A. Usafi wa mwili
- B. Mazingira machafu
- C. Umuhimu wa mazingira machafu
- D. Umuhimu wa mazingira safi.

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41hadi 50.

Siku moja paliishi mwindaji mmoja aliyekuwa hodari sana katika kazi yake ya kuwinda wanyama kama vile paa, swara, sungura, pofu na kadhalika. Mwindaji huyu alikuwa na mke na watoto wawili, mmoja wa kike na mwingine wa kiume. Wote walipendana kama chanda na pete. Watoto hawa waliipenda sana nyama ya swara kuliko nyinginezo zote.

Mtoto wa kiume aliitwa Bidii na ndiye aliyekuwa wa kwanza kuzaliwa naye wa kike Chaurembo. Bidii alifunzwa kazi ya kuwinda wanyama na baba yake ilhali Chaurembo naye akafunzwa kazi za nyumbani kama vile upishi, kufagia nyumba, kuosha nguo na vyombo, kuteka maji na utafutaji wa kuni. Mwalimu wake hakuwa mwingine ila mama yake.

Bidii naye kule msituni alikuwa mkali hata kushinda mwalimu wake. Hakukosa shabaha kamwe. Ungempa mishale mitano basi yote ingalirudi na wanyama watano. Kwa hivyo, Bidii angerudi nyumbani na wanyama kulingana na idadi ya mishale aliyopewa na baba yake.

Familia ya mzee huyo iliishi maisha ya raha mustarehe na hawakukosa chakula.

41. Familia ya mwindaji huyu ilikuwa na watu wangapi?
   A. Wanne. B. Watatu.
   C. Wawili. D. Watano.

42. Ni aina gani ya mnyama gani ambaye mzee hakuwinda?
   A. Swara. B. Ngiri.
   C. Paa. D. Pofu.

43. Ni mtoto yupi aliyefunzwa kuwinda wanyama?
   A. Chaurembo.
   B. Chaurembo na Bidii.
   C. Bidii.
   D. Wote wawili.

44. Bidii na Chaurembo walipenda sana nyama ya:-
   A. Sungura
   B. Pofu
   C. Paa
   D. Swara.

45. Ni kweli kuwa:-
   A. Bidii na Chaurembo hawakupendana
   B. Bidii alifunzwa kazi ya nyumbani
   C. Chaurembo na Bidii walipendana
   D. Chaurembo alikuwa mwindaji hodari.

46. Kati ya watoto hawa, ni nani alikuwa wa kwanza kuzaliwa?
   A. Bidii.
   B. Mwindaji.
   C. Chaurembo.
   D. Walizaliwa siku moja.

47. Familia hii iliishi kwa:-
   A. furaha
   B. huzuni
   C. woga
   D. hofu.

48. Kati ya kazi hizi, ni ipi Chaurembo hakufunzwa?
   A. Utafutaji wa kuni.
   B. Kuchota maji.
   C. Kupika chakula.
   D. Uchomaji wa makaa.

49. Bidii angepewa mishale miwili angerudi na wanyama wangapi?
   A. Watano
   B. Watatu
   C. Wawili
   D. Mmoja

50. Kichwa cha makala haya ni:
   A. Bidii na Chaurembo.
   B. Mke na watoto wawili.
   C. Wanyama pori.
   D. Familia ya mwindaji.

Compiled and supplied online by Schools Net Kenya | P.O. Box 85726 – 00200, Nairobi |
Mob. 0711 8822 27 | Email: infosnkenya@gmail.com | Order answers online at www.schoolsnetkenya.com